

Wewe ni mgeni uliyewasili kama mhamiaji au mkimbizi?

Je unahitaji msaada wa kupata huduma mbalimbali?
Unahitaji kufahamu huduma hizo zinatolewaje hapa
Australia?

Mshauri anaweza kukusaidia!

Mshauri ni mtu anayejitolea kutoka kwenye jamii ambaye amepata mafunzo ya kuwasaidia wageni wanaofika kama wahamiaji na wakimbizi kuweza kupata huduma na kuzitumia peke yao mara wanapohitaji.

Mshauri anaweza kutoa msaada pale unapohitaji kama ifuatavyo:

- Kwenda na wewe hospitali, kwa daktari wa magonjwa au daktari wa meno
- Kukuonyesha namna ya kutumia usafiri wa basi, treni na tramu
- Kwenda na wewe Centrelink kwa ajili ya ahadi ya kuonana
- Kufungua akaunti ya benki na kutumia mashine ya kutolea pesa (ATM)
- Kutafuta nyumba ya kupanga
- Kwenda na wewe maktaba na kupata kadi ya kutumia kwenye maktaba
- Kupata huduma za kuangalia watoto
- Kwenda na wewe ofisi za posta
- Kujifunza namna ya kutumia kompyuta
- Kuandaa barua ya kuomba kazi na pia kutafuta kazi

Kama unahitaji msaada kwa ajili ya huduma nyingine au ahadi za kuonana, au kuweza kujimudu hapa Australia, wasiliana na Whittlesea Community Connections kwa namba

9401 6666

[Ulizia Emma Antonetti, Dalal Sleiman au Grozda](#)

